


<p>6.Nyanya (Tomato)</p>	<p>-Twanga majani na mashina ya nyanya kiasi cha vikombe 2 na iache usiku kucha ikiwa ndani ya lita moja ya maji, chuja na ongeza nusu lita ya maji yenye povu la sabuni halafu nyunyizia mazao. - Chemsha majani na mashina ya nyanya yaliyokatwakatwa kiasi cha kilo moja ndani ya lita 2 za maji.....</p>	<p>Dawa hii inadhibiti wadudu kama vipepeo wa kabichi (cabbage butterfly) , viwavi na vidukari.</p>
<p>7.Lantana camara. 'akasheke la'</p>	<p>Kusanya majani ya Lantana, yakaushe kisha yaweke kwenye kifaa cha kuhifadhia nafaka-dawa weka chini na nafaka juu</p>	<p>Dawa inadhibiti wadudu kama <i>cassava weevil</i>, <i>grain weevil</i> nk</p>

<p>8.Jivu (wood ash)</p>	<p>Majivu yanaweza kutumika kama yalivyo au kwa kuchanganya na maji. Chukua kijiko kimoja cha chakula cha majivu , weka maji lita moja, subiri siku moja , chuja kisha changanya na kikombe kimoja cha chai cha maziwa halafu nyunyizia mazao. -Tandaza majivu juu ya ardhi karibu na mimea</p>	<p>Dawa hii inadhibiti wadudu wenye miili laini (soft-bodied insects) au wanaonyonya kama vidukari, vikata mimea,panzi, viwavi, mchwa, konokono nk Dawa hii hufukuza wadudu waharibifu kama minyoo, konokono, vikata mimea nk. Hali yake ya <i>alkaline</i> husababisha muasho mkali kwa wadudu.</p>
---------------------------------	---	--

MAYAWA- (Maendeleo ya Wakulima)
P.O.BOX 1753 - BUKOBA,TANZANIA (E-Africa)
TEL: +255 28 2220921
Mobile: +255 754 620794
Email: vanillaorganisation@yahoo.com
Website: www.mavicovanilla.com

MATUMIZI YA MADAWA YA ASILI



MAYAWA- (Maendeleo ya Wakulima)
P.O.BOX 1753 - BUKOBA,TANZANIA (E-Africa)
TEL: +255 28 2220921
Mobile: +255 754 620794
Email: vanillaorganisation@yahoo.com
Website: www.mavicovanilla.com

Aina ya dawa	Jinsi ya kuiandaa na kuitumia	Matumizi na maelezo mengine.
1. Pilipili (Chilli/ Red peppers)	Twanga kiganja kimoja cha pilipili iliyoiva kwenye kinu au ndani ya mfuko wa nailoni. Changanya na maji lita 4 na subiri kwa muda wa siku 1-3 au waweza kuchemsha kwa muda wa dakika 20. Changanya na povu la sabuni, chuja kisha nyunyizia mazao.	Dawa hii inadhibiti inzi weupe (white flies), konokono, vikata mimea (cut worms), <i>caterpillars</i> , <i>mealy bugs</i> nk.
2. Vitunguu maji, vitunguu swaumu na leaks (Onions, garlic and leaks)	Twanga majani ya vitunguu au vitunguu vyenyewe nusu kilo au kilo moja, changanya na maji lita 1-2 na subiri kwa muda wa siku 2-3 kisha chuja na changanya na maji yenye sabuni lita 2.	Harufu kali ya dawa hii itafukuza wadudu wafuatao: mchwa, vidugamba (<i>aphids</i>), viwavi wa aina mbali mbali nk.

3. Tumbaku (Tobacco)	<p>(a) Twanga majani ya tumbaku gramu 250, kisha changanya na maji lita 4, chemsha kwa muda wa dakika 20. Ikisha poa chuja na changanya na maji ya sabuni lita 5. Nyunyizia mazao.</p> <p>(b) Tandaza majani ya tumbaku karibu na mimea ili kuua au kufukuza wadudu waharbifu.</p> <p>(c) Unga wa tumbaku unaweza kuweka kwenye majani ya mimea iliyougua.</p>	<p>-Dawa hii inadhibiti wadudu wengi kama inzi wa aina zote, mchwa, vidugamba (<i>aphids</i>), viwavi wa aina mbali mbali, konokono nk.</p> <p>- Magonjwa ya kuku (fungal diseases) pamoja na bakteria yanaweza kuthibitiwa pia.</p> <p>NB: Uvunaji wa mazao ufanyike siku 4 au zaidi baada ya kunyunyizia dawa.</p> <p>: Usitumie dawa hii kwenye mimea jamii ya tumbaku (<i>Solanaceae family</i>)</p> <p>: Uwe mwangalifu maa-na tumbaku ni sumu kali sana kwa mifugo na binadamu.</p>
4. Mari-golds	-Twanga mmea mzima wa Marigold (majani, mizizi na maua). Chukua gramu 100-200 kisha changanya na maji moto lita moja na subiri kwa muda wa saa 24.	Dawa hii hudhibiti wadudu wengi kama minyoo wa ardhini (<i>nematodes</i>), inzi wa aina mbali mbali, vidukari (<i>aphids</i>), viwavi, <i>mites</i> nk.

	<p>Ongeza maji baridi kwa uwiano wa 1:1, chuja na nyunyizia mazao au nyunyizia udongo.</p> <p>-Sehemu yoyote ya mmea wa marigold ikikaushwa inasaidia kudhibiti wadudu ndani ya stoo (storage pests)</p>	Magonjwa ya kuku yanaweza kuthibitiwa pia.
5. Utupa (Tephrosia)	<p>-Twanga majani ya Utupa halafu changanya na maji katika uwiano wa gramu 100 za dawa kwa lita moja ya maji, subiri kwa muda wa saa mbili, chuja na changanya na maji ya sabuni halafu nyunyizia mazao</p> <p>- Twanga majani na vitumba (twigs) vya utupa, changany na maji katika uwiano wa 1:5, tumia dawa hii kuosha ng'ombe, mbuzi na kondoo</p> <p>-Twanga majani makavu ya utupa, chekecha halafu changanya na nafaka kama mahindi na maharage katika uwiano wa gramu 100 za unga wa utupa kwa kilo 100 za nafaka(1:1000)</p>	<p>Dawa hii hudhibiti wadudu kama mchwa, sisimizi, mbawakau (beetles), vidukari (<i>aphids</i>), vikatami mea, viwavi, inzi wa aina mbali mbali nk.</p> <p>Dawa hii inasaidia kudhibiti kupe, chawa na viroboto.</p> <p>-Dawa hii inasaidia kudhibiti wadudu kama dumuzi na <i>weevils</i> ndani ya ghala mpaka muda wa miezi mitatu.</p>